## CUF yahofia kunasa mtego wa vyama vya upinzani ..Uk.3

Mitandao @JAMVILAHABARI Jamvi la habari jamvihabari +255676807684 Email: jamvinews@gmail.com

GAZETI LAKO

# JAMVI LA HABARI

ISSN Na 2683 - 6548: Toleo Na. 2543 ALHAMISI MACHI 06, 2025 Bei Tsh. 1000 Kenya Ksh. 60 www.jamvilahabari.co.tz

# UJENZI BWAWA KIDUNDA WANOGA

- **Waziri** Mkuu Majaliwa aweka jiwe la msingi la ujenzi wake unaoleta matumaini makubwa likiwa na uwezo wa kuhifadhi maji lita bilioni 199
- **Linatajwa** kuwa suluhu ya changamoto ya maji Dar, Pwani na Morogoro, likiwa ni sehemu ya ndoto za hayati baba wa Taifa mwalimu Nyerere
- **Dk** Samia apongezwa kwa kujikita kutatua changamoto ya maji kwa vitendo Uk.2



*Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Waziri wa Maji, Juma Aweso wakiweka jiwe la msingi la ujenzi wa Bwawa la Kidunda wilayani Morogoro Vijijini, Machi 5, 2025. Kushoto ni Mbunge wa Nyasa, Mhandisi, Stella Manyanya, wa pili kushoto Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, Hamis Taletale na kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu)*

## Dk. Mpango ataka Afrika inufaike sekta ya nishati

Uk.3



# UJENZI BWAWA KIDUNDA WANOGA

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI MKUU, Kassim Majaliwa wa jana Machi 05, 2025 ameweka jiwe la msingi la ujenzi wa mradi wa Bwawa la Kidunda litakalokuwa na uwezo wa kuhifadhi maji lita bilioni 190 ambalo linatarajiwa kugharimu shilingi bilioni 335.8 hadi kukamilika kwake.

Akizungumza na wakazi wa kijiji cha Kidunda, Wilayani Morogoro, Mheshimiwa Majaliwa amesema kuwa ujenzi wa bwawa hilo ambao umefikia asilimia 28. Ujenzi huo ni utekelezaji wa maono ya Hayati baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere ambaye alidhamiria kulijenga ili kutatua changamoto ya upatikanaji wa maji kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro.

"Bwawa hili lilikuwa katika historia tangu Serikali ya awamu ya kwanza na zilizofuatia, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa dhamira yake ya kuhakikisha maji ya kutosha yanapatikana, alielekeza kuanza kutekelezwa kwa mradi huu, na leo tumeweka jiwe la msingi, na anamatarajio makubwa na mradi huu."

Mheshimiwa Majaliwa ameongeza kuwa ujenzi wa bwawa hilo ni utekelezaji wa dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha anamtua mama ndoo kichwani kwa kufikisha huduma ya maji safi na salama karibu na makazi ya wananchi.

Kadhalika Mheshimiwa Waziri Mkuu ameziagiza Mamlaka za Maji ziendelee kutoa elimu ya utunzaji wa vyanzo vya maji ili kuhakikisha miradi inayotekelezwa na Serikali kwa gharama kubwa iweze kuwa endelevu.

Pia, Mheshimiwa Majaliwa alisisitiza kuwa Wizara ya Maji ihakikishe inamsimamia mkandarasi ili mradi huo ukamilike kwa wakati "Tunataka mradi huu ukamilike kwa wakati, hatuna shaka na mkandarasi huyu, amefanya miradi mingi na kwa ufanisi".



# DK. MPANGO ATAKA AFRIKA INUFAIKE SEKTA YA NISHATI

NA MWANDISHI WETU

MAKAMU wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango ametoa wito wa kuimarishwa ushirikiano zaidi kwa Mataifa ya Afrika Mashariki ili kuweza kunufaika na sekta ya nishati ambayo inaendelea kukua kwa kasi.

Makamu wa Rais ametoa wito huo wakati akifungua Mkutano wa 11 wa Petroli wa Afrika Mashariki unaofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC) Jijini Dar es Salaam.

Amesema ni muhimu kuungana pamoja kuweza kutumia rasilimali iliyopo katika sekta ya nishati Afrika Mashariki na kutengeneza njia ya maendeleo endelevu na ustawi wa kudumu wa ukanda huo. Pia amewakaribisha wawekezaji na wadau wa maendeleo kuungana na Mataifa ya Afrika Mashariki katika kuendeleza sekta hiyo.

Makamu wa Rais amehimiza majadiliano katika Mkutano huo yaweze kusaidia katika sera za mataifa husika kwa maendeleo endelevu ya sekta ya nishati. Amesema ni lazima kuendelea kuhamasisha uhamaji wa haki kuelekea katika matumizi ya nishati safi na kuhakikisha athari za kiuchumi na kijamii za mabadiliko hayo zinakuwa sawa kwa watu wote na kila mmoja ananufaika na mabadiliko kuelekea matumizi ya nishati safi bila kuachwa nyuma.

Makamu wa Rais amesema ni muhimu kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kutumia kwa ufanisi rasilimali zote za nishati ikiwemo mafuta ili kuweza kukabiliana na upungufu wa nishati kutokana na kuongeza kwa mahitaji hayo katika kufikia maendeleo kwa haraka. Ameongeza kwamba rasilimali za nishati zitaweza kuwa chanzo kikuu cha mapato kwa serikali na hivyo kusaidia katika uwekezaji kwenye miundombinu na huduma za kijamii na kuunga mkono ajenda nzima ya maendeleo.

Amesema Afrika Mashariki imejaaliwa rasilimali kubwa ya nishati ikiwemo mafuta huku mataifa yakiwa na ugunduzi mbalimbali kama vile kugunduliwa kwa gesi asilia nchini Tanzania, mafuta nchini Uganda, Kenya na Sudan, Methane kwa nchi ya Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo pamoja na nishati ya jotoardhi kwa nchi za Tanzania na Kenya.

Halikadhalika Makamu wa Rais amesema maendeleo ya teknolojia ni fursa kwa nchi zinazoendelea kuongeza uwezo wa uvunaji endelevu wa nishati ya mafuta. Ameongeza kwamba ili na maendeleo endelevu ya sekta ya nishati ni muhimu mapato yanayotokana na uwekezaji huo yaweze kufadhili miradi mbalimbali ya maendeleo, kutengeneza ajira na uwekezaji katika jitihada za kurejesha mazingira yaliyoharibiwa. Amesema ni vema sera na sheria kujumuisha utengaji wa asilimia kadhaa ya mapato yatokanayo na rasilimali ya mafuta kwaajili ya matumizi ya baadae.

Kwa upande wake Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada za kuendeleza mkondo wa juu kwa lengo la kugundua na kuendeleza vyanzo vya gesi hapa nchini. Amesema katika uongozi wake kwa upande wa mkondo wa juu hatua muhimu imefikiwa ikiwemo kuimarisha uzalisha wa gesi asilia katika vitalu ya Songosongo na Mnazi bay ambavyo kimsingi ni maendeleo kwenye uchumi wa gesi.

Aidha Dkt. Biteko ameongeza kwamba maendeleo mengine ni pamoja na kuongezeka kwa ushiriki wa kampuni ya Serikali ya TPDC katika kitalu cha Mnazi bay kutoka ushiriki wa asilimia 20 hadi asilimia 40.

# WAZIRI MKUU AZUNGUMZIA NNYENZO YA KUPUNGUZA UMASIKINI

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI MKUU, Kassim Majaliwa amesema kuwa huduma jumuishi za kifedha ni kiungo muhimu cha ukuaji wa uchumi, kupunguza umasikini na kuchochea maendeleo ya jamii kwa ujumla.

Alisema Serikali kwa kutambua hilo imedhamiria kuendelea kushirikiana na wadau wote ili kuhakikisha sekta ya kifedha inazidi kuwa jumuishi, fanisi, na yenye tija kwa maendeleo ya Taifa.

Alisema hayo alipozindua huduma mpya za kidijitali za Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) katika ukumbi wa Super Dome, Masaki jijini Dar es Salaam.

Ameongeza kuwa katika vipindi tofauti, Serikali imekuwa ikiandaa na kutekeleza mikakati ya Taifa ya kuboresha huduma jumuishi za kifedha.

"Mpango Mkakati wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha wa 2023 - 2028 ni mwendelezo wa mafanikio yaliyopatikana kupitia Mpango Mkakati wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha uliokamilika Desemba 2022"

Kadhalika, Mheshimiwa Majaliwa alisema kuwa jitihada nyingine ni kuandaa Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali wa miaka 10 kuanzia mwaka 2024 hadi 2034. "Mkakati huu umeainisha malengo mahsusi ambayo kama nchi tunaazimia kuyatekeleza ili kufikia uchumi wa kidijitali."

Kwa upande wake, Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Sauda Msemo alisema sekta ya fedha imeendelea kuwa na ustahimilivu na hivyo kuwezesha shughuli mbalimbali za kiuchumi kufanyika.

Aidha, Naibu Gavana huyo ametoa wito kwa taasisi zote za kifedha zifuate viwango bora vya usalama wa mitandao na kugundua haraka pale panapotokea udanganyifu wa aina yoyote.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Theobald Sabi alisema lengo la uzinduzi wa huduma hizo za NBC kidijitali ni kuboresha utoaji wa huduma za kifedha na kuzifanya zipatikane kwa urahisi. "Huduma hizo ni pamoja na ufunguaji wa akaunti, kuhamisha fedha, kupata mikopo bila ya kwenda katika tawi."

Mradi huo utakapokamilika unatarajia Kuboresha huduma ya Majisafi kwa ajili ya matumizi ya Majumbani, Kilimo na Viwanda kwa kuhakikisha upatikanaji wa muda wote katika mto Ruvu kwa kutiririsha wastani wa lita 24,000 kwa sekunde zitakazokidhi mahitaji ya maji hususani kwenye kipindi cha ukame.

# MIKOPO UMIZA YAZIDI KUVUNJA NDOA MIJINI

NA MWANDISHI WETU

LICHA ya Serikali kupitia maeneo mbalimbali kukemea na kisha kuzuia wananchi kukopa pesa katika vikundi visivyosajiliwa, maarufu kama 'Mikopo Umiza', lakini kasi yake inazidi kuendelea na sasa imefikia hali mbaya zaidi.

Uchunguzi uliofanywa na gazeti hili umebaini kuwa familia nyingi kwa sasa zimetengana kutokana na kujiingiza katika mikopo hiyo ambayo baadaye husindwa kulipika na wadaiwa kuamua kutekeleza nyumba na kukimbia.

Madhila zaidi ya mikopo hiyo inaonekana katika miji inayokuwa kwa kasi Jijini Dar es salaam, ambapo ofisi nyingi ya mikopo ya aina hiyo inazidi kufunguliwa na kusababisha migogoro ya ndoa inayosababisha familia kusambaratika.

Imebainika kuwa waathirika wengi ni akina mama ambao huwa wanakopa bila kushirikisha waume zao na hivyo kulazimika kutoroka pale mambo yanapoharibika kwa kuhofia siri kufika kwa waume zao.

Miungoni mwa wahanga waliozungumza na gazeti hili katika maeneo ya Mbande Chamazi nje kidogo ya Jijini la Dar es salaam, wameweka wazi jinsi walivyoathiriwa na mikopo hiyo na kulazimika kuzikimbia nyumba zao.

Inaelezwa kuwa baadhi ya taasisi hizo za mikopo hutoa riba kubwa, mfano mtu anayekopa kiasi cha Shilingi Milioni moja, huanza kukatwa kodi mbalimbali na kukabidhiwa Laki Nane, lakini atatakiwa kulipa Shilingi Milioni moja na Laki nane kwa miezi sita!

"Tunalazimika kuwa wafanyakazi wa hizo taasisi kwa vile kila siku unatakiwa upeleke pesa na ukichelewa wanakufuata hadi sehemu unayofanyia biashara na kukudhalilisha" alisema Mama Lishe mmoja wa Chamazi Mbande.

Hata hivyo wanasema ni vigumu taarifa za utapeli huo kusikilizwa na vyombo vya usalama kwa vile mkopaji anaingia mkataba pasi kulazimishwa kutokana na ugumu wa maisha.

# CUF YAHOFIA MUUNGANO WA VYAMA VYA UPINZANI




NA MWANDISHI WETU

MWENYEKITI wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, amesema kuwa maridhiano ndani ya vyama vya upinzani yamekuwa yakileta madhara na kuwajeruhi, na kwamba wamejifunza kutokana na yaliyotokea kipindi cha nyuma.

Akizungumza na Wanahabari Lipumba amesema kuwa kuna watu wanaotafuta madaraka kwa maslahi binafsi badala ya kujenga demokrasia ya kweli.

Amesema kuwa mwaka 2020, alikumbana na hali ya kushangaza ambapo alijitokeza kugombea urais, lakini alikumbana na pingamizi la dakika za mwisho kutoka kwa Tundu Lissu, jambo ambalo alidai lilikuwa kinyume na misingi ya demokrasia.

Lipumba amesema kuwa ingawa alikamilisha taratibu zote za kisheria, alikumbana na kikwazo cha kisiasa kilichotokana na Mpinzani mwenzake ambaye alikuwa Mgombea Urais wakati huo kupitia Chadema Tundu Lissu

"Sasa ukishajua kwamba umegongwa, umeumwa lazima uwe na tahadhari, kuna watu ambao wanatafuta madaraka sio kujenga demokrasia.wapo kama Trump kwamba ukishaingia basi uanze kuwashughulikia wote, lazima tuwe macho katika hili kwa sababu tushagongwa gangwa sana" amesema Lipumba.

Prof. Lipumba ameongeza kuwa katika historia ya siasa za upinzani, vyama vimekuwa vikishirikiana kwa makubaliano ya muda mfupi, lakini mara nyingi hayo yamevurugwa kutokana na kutokuwa na umoja wa kweli. Akirejelea uchaguzi wa 2014, alikumbusha jinsi baadhi ya vyama vilivyokuwa vikitumia udhaifu wa vyama vingine kujinufaisha.

Amesisitiza kuwa ili kuhakikisha demokrasia inakua nchini, vyama vya upinzani vinapaswa kuwa na maridhiano ya kweli na ya kudumu, badala ya kuingiza maslahi binafsi katika vikao vyao.

"Mifumo isiyo huru tulikubaliana kabisa sasa mnafanyeje pasina kuwa na maridhiano, sasa ukiwa unahitaji unatoa wito kwamba tufanye maridhiano, tufanye mazungumzo tukae katika kikao cha pamoja.sasa ikiwa ndo wito wako huo ukaweka tu kama hatukai kwenye kikao cha pamoja hili na hili, moja kwa moja unaonekana kwamba hauhitaji kuwa na maridhiano."

"Katika masuala ya kidiplomasia inabidi nondo zako zingine uziweke akiba. kama utakwenda na kauli mbiu kwamba tutaicheza ngoma kwa Kadri itakavyodundwa basi hiyo msitoe mapema iweke akiba.lakini pia uwaandae watu" amesisitiza Lipumba

# BITEKO: UMEME NDIYO NJIA KUBADILISHA UCHUMI



NA MWANDISHI WETU

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko amesema kuwa nishati ya umeme siyo anasa katika maisha ya watu bali itakuwa ndio injini ya kwanza ya kubadilisha uchumi wa nchi na maisha ya watanzania kwa ujumla.

Dk. Biteko ameyasema hayo jijini Dar es Salaam wakati wa kongamano la kuhamasisha matumizi ya nishati ya kupikia kwa umeme lililoandaliwa na Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco). Biteko amesema ni ukweli uliyowazi kuwa umeme siyo anasa bali ni injini ya kubadilisha uchumi hivyo anawaomba wanawake hasa wa Tanesco kuambiana ukweli na kumkemea mtu yeyote miongoni mwao anayemtafuta mteja na kumuomba rushwa ili amuunganishie umeme.

"Tuwakemee watu hawa kwa nguvu zetu zote ili watanzania wapate umeme wa uhakika kwa sababu serikali yao inawekeza fedha nyingi kwa ajili ya kuwapatia umeme, ninaamini wakinamama wakiamua katika shirika hili tutakuwa na shirika bora," amesema Dk. Biteko

Aidha amewataka wanawake waliopo Tanesco kuwa wa kwanza kubadilika kabla ya watu wengine kwa kutumia nishati safi ya kupikia ya umeme.

"Siku moja nitaamua kumtembelea mmoja wa watumishi ili kuona mnapikaje huko je mnatimua majiko ya umeme, si huwa mnaodha na kuodhesha kwenye sherehe zenu, msishangae nikaja na kupitiliza hadi jikoni kuangalia mnapikaje, maana tusihubiri injili ambayo sisi hatuiishi, tuanze sisi kupikia nishati safi nak ama jiko kwako una mbadala wa mkaa toa tafuta mkaa mabadala," amesema Biteko

Dkt. Biteko amesema kuna baadhi ya watu wanaamini kupika kwa kutumia umeme ni gharama kubwa hivyo umeme kazi yake ni kuzima na kuwasha taa tu, jambo ambalo amesema si kweli hivyo watanzania wanapaswa kuondokana na dhana hiyo.

"Niwatoe wasiwasi kuna majiko mbalimbali sasa hivi ambayo yanatumia umeme ambapo Unit moja unaweza kupikia kwa zaidi ya saa moja ambayo thamani yake haizidi Sh. 350. Hivyo tutaendelee kutoa elimu kwa jamii kuwa nishati ya umeme ni nafuu na rahisi kutumia," amesema

Hata hivyo Dk. Biteko amesema kuwa kupitia mfuko wa Nishati safi ya kupikia, Serikali itahakikisha kuwa wanawake wanapata mikopo yenye riba nafuu ili waweze kushiriki kikamilifu katika biashara za nishati safi. Pia, Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa Sera na Sheria mbalimbali zinakuwa rafiki kwa wawekezaji wa nishati safi ya kupikia ili waweze kushiriki kikamilifu katika biashara ya nishati safi ya kupikia.

Aidha Dk. Biteko ampongeza Mkurugenzi wa Tanesco kwa kuanza kutoa fursa sawa kwa wanawake kushika nafasi za juu za uongozi ndani ya Tanesco kwani kwa muda mrefu nafasi za juu za uongozi hasa wakurugenzi katika shirika hilo zimekuwa zikishikwa na wanaume.

"Katika wakurugenzi wote waliopo Tanesco 12 kati ya hao wanne ni wanawake, nimpongeze Mkurugenzi wa Tanesco katika hili kwa kuanza kutoa fursa sawa, hata hivyo bado tunakazi ya kufanya ya kuhakikisha tunatoa fursa kwa wanawake kushika nafasi za juu za uongozi," amesema.

Naye, Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga amewataka watanzania hususan wanawake kuendelea kuiunga mkono ajenda ya matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa kutumia na kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa watanzania wote.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Gissima Nyamo – Hanga amesema kuwa Serikali imeweka msukumo katika matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa kutumia nishati ya umeme kwa kuwa ni nafuu zaidi na imefika kila mahali nchini.

Amesema ni muhimu wananchi wakatumia majiko ya umeme ili waweze kuokoa muda na kwamba ajenda ya nishati safi ya kupikia ni ya kipaombele na imezungumzwa sana hivyo Tanesco inayowajibu wa kuhakikisha ajenda hiyo inatekelezwa.

Aidha, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TANESCO, Balozi Zuhura Bundala amesema kuwa wanawake ndio wahusika wakuu wa matumizi ya nishati safi ya kupikia. Amesema nishati safi ya kupikia ina gharama nafuu na ni rahisi kwa matumizi.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma Tanesco, Irene Gowelle amesema kuwa kongamano hilo ni la kihistoria na la kwanza kufanyika kwa ukubwa hapa nchini likiwa na lengo la kuhamasisha watanzania kutumia nishati safi ya kupikia ya umeme.

"Kongamano hili litakuwa sehemu ya watu kujifunza na kupeleka mbele ajenga ya kuhamasisha watanzania kutumia nishati hii safi ya kupikia ya umeme kwa vitendo," amesema Gowelle

Jukwaa hilo limelenga kuhakikisha kwamba kila Mtanzania, hususani mwanawake, anapata fursa ya kutumia nishati safi kwa kupikia.

# MAMA MWINYI ASHAURI WAZEE NA WATOTO WASAIDIWE




NA MWANDISHI WETU

MKE wa Rais wa Zanzibar, Msarifu na Mwenyekiti wa Bodi ya wadhamini ya Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation (ZMBF), Mhe.Mama Mariam Mwinyi ametoa rai kwa wadau mbalimbali kuwasaidia Watoto na Wazee wenye mahitaji Maalum katika kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Mariam Mwinyi aliyasema hayo alipovitembelea Vituo vya kuwalea Watoto SOS, Mazizini na cha Wazee Welezo kuwapa msaada wa vyakula, Mkoa wa Mjini Magharibi jana.

Aidha, Mariam Mwinyi ameeleza kuwa ataendelea kuwasaidia zaidi Watoto na Wazee wenye mahitaji Maalum ikiwemo vyakula katika kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na Sikukuu ya Eid.

Mariam Mwinyi amewahimiza Watoto kuwa wenye tabia njema na kufanya ibada katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani .

Halikadhalika Mama Mariam Mwinyi amewasilisha salamu za upendo kutoka kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt.Hussein Ali Mwinyi katika vituo hivyo.

Naye, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Wazee na Watoto Zanzibar Mhe. Dkt.Riziki Pembe Juma amemshukuru Mama Mariam Mwinyi kwa kuendelea kuwajali Watoto wenye mahitaji Maalum katika vituo mbalimbali Zanzibar.


# TANGAZA NASI SASA

*Unatamani kukuza biashara yako kutoka hapo ilipo kuwa kubwa na yenye mantiki zaidi?*

- *Unatamani kuongeza kipato, uelewa na upana wa shughuli zako za kila siku?*
- *Je unataka kuwafikia wateja wako ndani na nje ya nchi kwa kiasi kikubwa ili kukuza biashara na huduma yako?*
- *Fahamu kwamba JAMVI LA HABARI na mitandao yake ya kijamii kama Youtube, Instagram, Facebook, Website na Twitter hutembelewa na maelfu ya wasomaji kila siku Duniani kote.*
- *Hivi unafahamu kuwa JAMVILAHABARI kwa sasa ni moja kati ya Media chache zinazo ongoza kwa kutoa taarifa sahihi na kwa wakati zinazotokea nchini na Duniani kwa ujumla?*

*TANGAZA SASA NA JAMVI LA HABARI KWA PUNGUZO KUBWA LA BEI UPATE MATOKEO YA HARAKA.*

*Kwa matangazo yote kama vile minada, kupotelewa kwa vyeti vya shule, matangazo ya makampuni, nafasi za kazi, zabuni za kazi, maonyesho, dawa za asili, taasisi za elimu, taasisi za dini na mengine mbalimbali mbali mbali.*

*Ni rahisi sana, wasiliana nasi kupitia Whatsap namba +255659555744 au tupigie katika +255743777778 au +255659555744 GHARAMA ZETU NISAWA NA BUREE JAMVILAHABARI; TUMECHAGUA KUKUHUDUMIA www.jamvilahabari.co.tz*

# SHIRIKA LA WORLD VISION YAIPIGA SHINYANGA

NA MWANDISHI WETU

SHIRIKA la World Vision Tanzania limekabidhi vifaa vyenye thamani ya shilingi milioni 97.6 kwa serikali ya mkoa wa Shinyanga ikiwa ni sehemu utekelezaji wa mradi wa NOURISH unaotekelezwa wilayani Kishapu.

Vifaa hivi vinajumuisha mizinga ya nyuki, pampu za umwagiliaji, mbegu za mazao, mashine za kukamulia asali, na vifaa vya kuhifadhi mazao, vyote vikiwa na lengo la kuboresha uchumi wa kaya, lishe ya familia, na kuongeza uzalishaji wa mazao katika kata za Lagana, Ngofila na Mwamashele wilayani Kishapu.

Hafla ya makabidhiano imefanyika Februari 4, 2025 mjini Shinyanga, ambapo Mgeni Rasmi, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Mhe. Anamringi Macha, ameongoza tukio hili muhimu.

Vifaa vilivyokabidhiwa vinategemewa kusaidia wakulima na familia katika wilaya ya Kishapu, ikiwa ni juhudi za pamoja kati ya shirika la World Vision na serikali ya mkoa katika kuboresha hali ya maisha, hasa kwa watoto na familia zinazokabiliwa na changamoto za lishe na upatikanaji wa chakula.

Muonekano wa sehemu vifaa vilivyotolewa na Shirika la World Vision Tanzania

Kaimu Meneja wa World Vision Tanzania Kanda ya Ziwa, Shukrani Dickson, ameeleza kuwa, Vifaa vilivyokabidhiwa ni sehemu ya juhudi za shirika kuboresha upatikanaji wa chakula na lishe bora kwa familia, hasa watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Amefafanua kuwa vifaa hivyo vimetolewa kupitia mradi wa NOURISH unaofadhiliwa na nchi ya Ireland. Mradi huu unafanya kazi ya kuboresha lishe, uzalishaji mali na kuongeza kipato kwenye kaya pamoja na kuwezesha jamii kupata elimu ya kukabiliana na maafa katika Wilaya ya Kishapu, kwa kushirikiana na Shirika la KIVULINI ambao wanafanya kazi katika sekta ya usawa wa kijinsia.

Kaimu Meneja wa World Vision Tanzania Kanda ya Ziwa, Shukrani Dickson (katikati) akimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Mhe. Anamringi Macha vifaa mbalimbali vya Kilimo, ufugaji nyuki na lishe kwa ajili ya kuboresha uchumi wa kaya na lishe wilayani Kishapu

Ameeleza kuwa , vifaa vilivyokabidhiwa vinajumuisha Mizinga ya nyuki, vifaa vya kurinia asali na mashine ya kukamulia asali, mifuko ya kinga njaa, pampu za umwagiliaji, mbegu za mboga mboga na mazao, mbolea za kupanda na kukuzia, miti ya matunda, mashine ya umeme ya kukaushia mazao ya mbogamboga na vifaa vya kujengea friji ya asili ya kutunza mazao ya mbogamboga vyenye thamani ya shilingi 97,649,200/= vyote vikiwa na lengo la kuboresha kilimo na kuongeza tija katika uzalishaji wa chakula.

"Mradi huu ni muhimu sana kwa sababu unalenga kuhakikisha jamii yetu inapata chakula cha kutosha na bora, na pia tunawawezesha wanawake na vijana kupitia shughuli za kilimo na biashara ya mazao," amesema Shukrani.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Mhe. Macha, amelishukuru shirika la World Vision kwa mchango wake, akisema kuwa vifaa hivi vitasaidia sana katika kuboresha uchumi wa wananchi na kuongeza tija katika sekta ya kilimo.

"World Vision Tanzania ni taasisi inayotoa michango yenye mashiko na manufaa kwa jamii. Tunashukuru kwa namna inavyoshirikiana na serikali kuboresha maisha ya wananchi. Shukrani za pekee ziende kwa Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake mzuri ambao umeweka mazingira rafiki kwa wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi kufanya shughuli zinazolenga kuwaletea maendeleo wananchi," amesema Mhe. Macha.

Amewataka wakulima na wananchi kutumia vifaa hivi kwa manufaa yao, na ameahidi kutembelea kata za Lagana, Mwamashele, na Ngofila ili kujionea maendeleo yatakayopatikana kutokana na vifaa hivi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Mhe. Peter Masindi, amesema kuwa vifaa hivi vitachochea maendeleo na kuleta mapinduzi katika kilimo cha kibiashara katika wilaya hiyo.

Ametoa wito kwa wadau wengine kuendelea kushirikiana na serikali ili kuhakikisha wananchi wanapata fursa za kiuchumi.

Wanufaika wa vifaa hivi wameeleza shukrani zao kwa World Vision na serikali kwa ushirikiano wao, wakiahidi kutumia vifaa hivyo kujiletea maendeleo na kuboresha maisha yao.

Shirika la World Vision Tanzania linajivunia miradi yake inayotekelezwa katika mikoa mbalimbali ya Tanzania, likifanya kazi kwa karibu na jamii na serikali katika kuboresha huduma za afya, elimu, lishe, uzalishaji mali, na haki za kijinsia.

Katika mkoa wa Shinyanga Shirika la World Vision lina miradi katika wilaya 3 za Shinyanga, Kishapu na Kahama likishirikiana na serikali na jamii kutoa huduma za jamii. Miradi hiyo ni Mpango wa Eneo Kilago uliopo Kahama, Mpango wa eneo Mwakipoya, Mpango wa eneo Lagana, Mradi wa NOURISH upo Kishapu na GROW ENRICH inafanya kazi katika wilaya mbili za Kishapu na Shinyanga.

Shirika la World Vision Tanzania ni Shirika la Kikristo la maendeleo, misaada na utetezi, lisilo la kiserikali ambalo limejikita kufanya kazi na watoto, familia, na jamii ili kupambana na umasikini na ukosefu wa haki.



# TAHARIRI

## Nida iondoe usumbufu Ugawaji wa vitambulisho

KWA siku za hivi karibuni vituo vya NIDA katika miji na mikoa mbalimbali vimekuwa vikishuhudiwa msongamano mkubwa wa wananchi wanaoshinda hapo kuanzia asubuhi mpaka majira ya jioni, ofisi zinapofungwa.

Wanachofuata katika ofisi hizo ni utekelezaji wa agizo la Mamlaka ya hiyo iliyowataka wananchi wafuatilie vitambulsho vyao, vinginevyo watasitisha matumikzi ya namba.

Kinachoonekana ni kutokuwa na maandalizi ya uhakika kwani idadi kubwa ya wananchi wanapofika katika ofisi hizo, wamekuwa wakikumbana na usumbufu kutoka kwa walinzi na hata mzunguko unaotakiwa kuufuata kabla ya kuelekezwa namna ya kupata kitambulisho.

Sisi tunaona kuwa njia ile ya awali ya kupeleka vitambulisho katika ofisi za Serikali za Mitaa ilikuwa muafakja lakini ilikikosa uratiubu mzuri.

Katika maeneo mengi ya serikali za mitaa tulikuwa tukishuhudia maelekezo ya uwepo wa vitambulisho vya wananchi lakini walipokuwa wakivifuata hata kama maelekezo yanaonyesha vilikuwepo ofisi husika lakini havikuwepo.

Wananchi wengi walijikuta wakitembea kila kata kutafuta vitambulisho vyao bila kupatikana jambo ambalo liliwakatisha tamaa wengi na kukuta vitambulisho vilivyostahili kuwa huku vimepelekwa kule.

Sisi tunadhani njia ya kurudisha zoezi hilo katika ofisi kuu za NIDA ni nzuri, lakini lingeratibiwa vizuri na kuondoa urasimu ili zoezi liende sawia.

Aidha kurudisha maeneo ya aina hiyo kwa namna moja au nyingine itachochea kutokea vitendo vya kuomba rushwa kwa vile wananchi wengi  hawapendi kupoteza muda katika jambo wanaloweza kulifanya kwa kutoa rushwa.

Tunadhani itakuwa ni wakati mzuri kwa Mamlaka, kuliangalia tena zoezi hili na kisha kuamua kufanya mawili, au kuboresha ofisi za Serikali za Mitaa na kata au kuweka mazingira mazuri katika ofisi kuu za NIDA.


## BODI YA UHARIRI

Mhariri Mkuu - 0762 178 678
Idara Ya Matangazo/Masoko - 0743 777 778, - 0659 555 744
Idara Ya Usambazaji - 0676807684, - 0787 288 160

Gazeti hili hutolewa na **JAMVI MEDIA GROUP**
S. L. P 78862, Dar es Salaam
**Tel:** +255 676 807684, 255 743 777778
**Email:** jamvinews@gmail.com
www.jamvilahabari.co.tz




*Waziri wa Ujenzi, Abdallah Ulega (kulia) akizungumza na mkandarasi katika moja ya miradi ya ujenzi aliyotembelea jijini Dar es Salaam jana na kubaini upungufu mkubwa wa utendaji na kufuata mikataba.*

UCHAMBUZI

## Serikali yasisitiza nidhamu miko ya halmashauri

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, ametoa onyo kwa wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi endapo itabainika kuwa vikundi hewa katika maeneo yao vilivyonufaika kupitia mikopo ya asilimia 10, watawajibishwa.

Waziri Mchengerwa ametoa onyo hilo jijini Dodoma wakati wa hafla ya utiaji saini mikataba ya utoaji mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulamavu kati ya halmashauri 10 na benki mitatu.

Amewataka Mkuu wa Mkoa , Wilaya na Wakurugenzi wafuatilie kwakuwa hataki kusikia vikundi hewa. "Nawambia wazi kabisa, tumefika hapa kwasababu kuna watumishi wasio waaminifu ambao walitafuna fedha hizi kwa kukopeshana wenyewe na hawakuwa na sifa ya kupokea mikopo hii."amesema Mchengerwa

Aidha Mchengerwa amesisitiza kuwa uadilifu kwenye fedha hizo na kuwataka wafuatilie vikundi vyote na kuvijua na asisikie vikundi hewa.

"Fedha hizi ni za moto wajibu wetu ni kumsaidia Rais fedha hizi zisiende kuchezewa, naelekeza kikundi hewa kitakachobainika eneo lolote viongozi wa eneo hilo mtapaswa kuwajibika, tumieni vyombo mnavyosimamia kwenye mikoa na wilaya kuhakikisha hakuna vikundi hewa, fedha zisimamiwe na kurejeshwa."amesisitiza

Hata hivyo amesema vikundi vyote vinavyopokea mikopo hiyo vinatakiwa kufanya shughuli za uzalishaji na kurejesha fedha kulingana na mipango ya marejesho.

"Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi tumekubaliana jukumu la usimamizi wa fedha hizi ni la kila mmoja wet una wakati tunamshauri Rais sisi Wizara tulimhakikishia kuanzia kwangu kwamba iwapo kutakuwa na kulegalega kukote mimi na wasaidizi wangu tutalazimika kuwajibika."

Amesema Benki ya NMB itafanya kazi kwenye halmashauri za wilaya za Bumbuli, Itilima, Newala, Manispaa ya Songea, Jiji la Dodoma huku benki ya CRDB itafanya kazi Wilaya za Nkasi, Mji wa Mbulu, Manispaa ya Kigoma na Jiji la Dar es salaam.

Hata hivyo, amesema Benki ya Biashara ya Uchumi itafanya kazi Halmashauri ya Wilaya ya Siha.

"Zaidi ya Sh.Bilioni 234 zinakusudiwa kupelekwa kwa wananchi kwa njia mbili za utoaji mikopo hiyo ambazo ni kupitia Benki kwa Halmashauri 10 na mikopo iliyoboreshwa kwenye Halmashauri 174.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Tamisemi, Profesa Adolf Ndunguru amesema kuwa kusainiwa mikataba hiyo ni mwanzo wa mapinduzi ya kuhakikisha mikopo hiyo ya asilimia 10 inakuwa na tija tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma.

# Wanawake watakiwa kuji

NA MWANDISHI WETU



KATIBU Tawala Wilaya ya Kahama Bi. Glory Absalum amewasihi wanawake na wananchi wote wa kushiriki kikamilifu katika Maadhimisho ya siku ya Wanawake Duniani kwani watapata fursa ya kutembelea kwenye mabanda na kupata huduma mbalimbali za kijamii pamoja na kupata fursa ya kuuza na kununua bidhaa ikiwa ni sehemu ya kusherehekea juhudi za Serikali za kuimarisha haki usawa na uwezeshaji.

Ametoa wito huo leo Machi 4, 2025 wakati wa Uzinduzi wa Maadhimisho ya Siku ya Mwanamke Duniani yanayofanyika kwenye Kata ya Bugarama, Halmashauri ya Msalala Wilaya ya Kahama ambapo pia amesema Kaulimbiu ya mwaka huu inatoa mwaliko kwa watu wote kushiriki katika maadhimisho haya kuhakikisha kuna haki, usawa na uwezeshaji.

"Ninawasihi wanawake na wananchi wote kujitokeza kushiriki kikamilifu katika Maadhimisho ya Siku ya Wanawake kwani mtapata fursa ya kutembelea kwenye mabanda na kupata huduma mbalimbali za kijamii ikiwa ni sehemu ya kusherehekea juhudi za Serikali za kuimarisha haki, usawa na uwezeshaji", amesema Bi. Glory.

AIdha amewasihi wanawake kuendelea kutumia nishati safi ya gesi kwa ajiri ya kupikia ili kuunga mkono juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha kuna matumizi makubwa ya nishati safi yakiambatana na utunzaji salama wa mazingira.

Maadhimisho ya Siku ya Mwanamke Duniani kwa Mkoa wa Shinyanga yanaadhimishwa kwa siku tatu kuanzia leo Machi 4 hadi Machi 6 katika Kata ya Bugarama, Halmashauri ya Msalala Wilaya ya Kahama yenye Kaulimbiu "Wanawake na Wasichana 2025: Tuimarishe Haki, Usawa na Uwezeshaji"

Sherehe za kitaifa za siku hiyo ya Wanawake duniani hapa nchini itafanyika jijini Arusha ambapo hivi karibuni Wanawake zaidi ya 300 walijitokeza kufanya usafi katika Jiji la Arusha ikiwa ni Hamasa kwaajili ya siku ya wanawake Duniani utakayofanyika kitaifa 8Machi 2025 ambapo Rais w Jamhuri ya Muun gano wa Tanzan Dkt.Samia Suluh Hassan anatazam wa kuwa mge Rasmi

Akizungumz mwenyekiti w Kamati ya maan dallizi ya Hamas Hindu Bweng alisema kuwa maa dhimisho hayo y takuwa ya tofau na ilivyozowelek

# toa kuadhimisha siku yao



> Hii ni fursa muhimu ya kuonyesha juhudi za wanawake katika maendeleo na kujenga jamii yenye usawa wa kijinsia. ambapo Maadhimisho..

Amani kutoka Ofisi ya Mkuu wa mkoa, uwanja wa Shekhe Amri Abeid Soko la Kilombero na kumalizikia uwanja wa Ngarenaro ambapo michezo mbalimbali ya wanawake itakapofanyika huku akiwataka wanawake kujitokeza kwa wingi siku hiyo

Kwa upande wake mwenyekiti wa Kamati ya michezo Diana Moshi alisema kuwa maadhimisho hayo yatakuwa na michezo ya aina mbalimbali, ikiwa ni pamoja na mchezo wa asili wa mdako, Rede, mechi za mpira wa miguu kati ya timu maarufu za wanawake, Simba Queens, Yanga princess, JKT Queens na Fountain Gate FC, ili kusherehekea ushiriki wa wanawake katika michezo.

"Mdako ni mchezo asilia wa watoto wa wa Afrika Mashariki wa Mchezo huu unashirikisha watoto wawili na kuendelea ambao hutumia vijiwe au changarawe kumi na mbili ambapo Kati yake moja huteuliwa kuwa malkia Mwenye zamu hulichukua na kulirusha juu na kuanza kuchambua yaliyobakia katika duara dogo au shimo akianza na mojamoja, kisha mawilimawili na kuendelea. Mshiriki anayefanikiwa kuchambua mawe yote bila kudondosha malkia huwa mshindi.

"IPO michezo mingi utakayofanyika kabla ya kufikia kilele chenyewe , hivyo Nawaomba wanawake kunitokeza kwa wingi mchezo kama wa rede, Mdako, kuvuta mamba na mingine mingi mama usibweteke njoo kwani maadhimisho yanawaleta wanawake pamoja na kuondoa tofauti zetu. Alisema.

Kwa upande wake Afisa Elimu Mkoa wa Arusha Sara Mlacky aliwataka wanawake kuhakikisha watoto ambao hawajaadikishwa kwaajili ya kuanza shule wafanye hivyo kwani ni katika kuwapatia haki yao ya msingi ya Kupata Elimu na kuwajengea msingi bora.

Aidha kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa wa Arusha Christian Paul Makonda, Mkoa huo utakuwa mwenyeji wa sherehe kubwa za kuadhimisha Siku ya Wanawake ambapo kwa mara ya kwanza, maadhimisho haya yatakuwa ya kipekee, ambapo sherehe zitaanza tangu Machi 1, 2025, na kudumu kwa siku saba, ikiwa ni sehemu ya Wiki ya Mwanamke, Katika kipindi hicho, wizara nane zitatoa huduma muhimu kwa jamii, ikiwa ni pamoja na huduma za afya, kisheria, na elimu ya fedha.

"Hii ni fursa muhimu ya kuonyesha juhudi za wanawake katika maendeleo na kujenga jamii yenye usawa wa kijinsia.ambapo Maadhimisho hayo yatalenga kuhamasisha usawa wa kijinsia na kutambua mchango mkubwa wa wanawake katika nyanja mbalimbali za jamii."

awali, kwani shughuli zitaanza tangu Machi 1, 2025,hivyo amewataka wanawake kujitokeza kwa wingi kushiriki kikamilifu.

Vilevile Bi Hindu alisema maandalizi yanaendeleea vyema, huku akianisha maeneo waligofanya usafi kwani walianza. Maandamano ya



# NLD YAIFUATA CCM KUSHIRIKI UCHAGUZI MKUU




NA MWANDISHI WETU

CHAMA cha National League for Democrats (NLD), kimetangaza kuanza kwa mchakato wa ndani ya chama wa kuwapata wagombea wa nafasi za Udiwani, Ubunge na Rais kuelekea Uchaguzi Mkuu, utakaofanyika mwezi Oktoba mwaka huu.

Aidha chama hicho kimetangaza neema kwa wagombea wanawake, kuwa hawatotoa ada yoyote wakati wa kuchukua fomu, lengo ni kuwapa fursa ya kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi za uongozi.

Akizungumza mapema leo na waandishi wa Habari, Katibu mkuu wa NLD Taifa ,Doyo Hassan Doyo, amesema, chama hicho kimelenga kusimamisha wagombea katika majimbo yote ya Uchaguzi kuanzia Udiwani, Ubunge pamoja na nafasi ya Rais,

"Chama chetu kitashiriki Uchaguzi Mkuu, hivyo kwakutambua hilo, leo tunatangaza rasmi kuwa ,chama kimefungua milango ya kuanza mchakato wa kuwapata wagombea wa nafasi za Udiwani, Ubunge na Rais, hivyo watu wote wenye sifa wanakaribishwa kushiriki, ili ukidhi sifa ya kushiriki mchakato huu ni lazima uwe Mwanachama hai wa Chama chetu," aliongeza Doyo Doyo alisema kuwa, kwaupande wa wagombea Wanawake hawatolipa ada yoyote wakati wa mchakato wa kuchukua fomu,

"Chama chetu, kwa mapenzi mema kabisa, na kwakuona umuhimu wa akinamama, tumeamua kuwa, wanawake wote watakaojitokeza kugombea nafasi za uongozi ndani ya chama chetu, hawatolipa ada yoyote ya fomu, hii itasaidia kuongeza hamasa na kujitokeza kwa wingi kuwania nafasi za Udiwani, Ubunge na Rais"Alisisitiza Doyo

Aliongeza kuwa katika kikao cha Kamati Kuu ya Chama hicho Februari 23, mwaka huu, chama hicho kilianzimia kuwa kabla ya Uchaguzi Mkuu ni lazima kufanyike mikutano ya hadhara na ndani ili kupata wagombea wenye uwezo pamoja na Tume ya Taifa ya Uchaguzi 'INEC' nilazima iweke wasimamizi wa Uchaguzi wenye weledi, ili uchaguzi uwe huru na haki.

Hicho ni chama cha pili cha siasa kilichotangaza kushiriki uchaguzi Mkuu kabla ya hapo CCM ambacho ni chama tawala nacho kilithibitisha kushiriki tukio hilo la kikatiba.

Hivi karibuni Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na Mgombea Mwenza wa Urais Tanzania Bara, Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, amewahimiza wanachama wa Jumuiya ya Umoja wa Wazazi kuendelea kujipanga vyema ili kuhakikisha chama kinashinda Uchaguzi nafasi za Ubunge na Udiwani kwa kuzingatia sera na maadili.

Ilikuwa ni katika kikao cha Kamati ya Utekelezaji ya Jumuiya hiyo jijini Dodoma, Dkt. Nchimbi alisisitiza kuwa CCM ni chama kinachojikita katika sera na maendeleo, si katika matusi au kejeli.

"Chama chetu kimefanya mambo makubwa kwa maendeleo ya taifa. Tunapaswa kuendelea kusimamia hoja zenye mashiko na si kutumia lugha zisizofaa. Tunapaswa kuwa mfano wa kuheshimu watu na kuzungumzia maendeleo yanayoonekana," alisema.

Aidha, alieleza kuwa serikali inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanikisha mambo mengi ambayo yanaweza kuwahamasisha wananchi kuendelea kukiamini chama.

"Tunayo mengi ya kuwaambia Watanzania kuhusu maendeleo yaliyofikiwa, hatuna sababu ya kutumia lugha za kejeli. Hayo tuwaachie wale wasiokuwa na hoja za msingi," aliongeza.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Wazazi Taifa, Fadhili Maganya, alisema kuwa ujio wa Dkt. Nchimbi katika kikao hicho ni ishara ya heshima kwao.

"Uwepo wako hapa umetupa faraja kubwa. Tumekukaribisha ili usikilize mawazo yetu na kutushauri. Hii ni historia, kwani sisi ndiyo jumuiya ya kwanza kuketi na wewe tangu uteuliwe kuwa mgombea mwenza," alisema Maganya.

Kikao hicho kilitoa fursa kwa viongozi wa Umoja wa Wazazi kujadili masuala muhimu yanayohusu ustawi wa jumuiya na mchango wake katika mustakabali wa chama kuelekea uchaguzi ujao.

Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi aliyasema haya kwenye Kikao cha Kamati ya Utekelezaji ya Baraza Kuu la Umoja wa Wazazi, Jumuiya ya CCM, ambacho alialikwa na kushiriki akiwa mgeni maalum, leo Jumamosi tarehe 8 Februari 2025, katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete, jijini Dodoma.

"Katika kikao chetu cha hivi karibuni, chama chetu kiliazimia kuwa ni lazima tufanye mikutano ya hadhara kwakipindi hiki ili tupate wagombea wenye uwezo, lakini pia kwa upande wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi 'INEC' ni lazima iweke wasimamizi wa Uchaguzi wenye weledi ili Uchaguzi uwe huru na haki, na usiwe na dosari," alisisitiza Doyo

# LIFAHAMU ENEO HATARI KWA UKATILI KWA WANAWAKE

NA MWANDISHI WETU

NEW Guinea kaunti ya Papua inatajwa kuwa ni moja ya sehemu hatari zaidi hapa duniani kwa wanawake kuishi kutokana na ukatili unaofanyika dhidi ya wanawake kwani asilimia 70 ya wanawake waishio mji huo hubakwa.

Katika mji huo wanaume wanaamini kuwa kumfanyia ukatili mwanamke ni jambo la kawaida ambalo linakubalika kwa kile walichodai kuwa ili mwanamke aweze kumtii mwanaume, ni lazima afanyiwe ukatili kwa kupigwa, kubakwa au kukatwa baadhi ya viungo vya miili yao kama vile masikio na kadhalika.

Polisi wa jiji hilo walihojiwa juu ya ukubwa wa tatizo la ukatili wa jinsia katika mji huo na kusema kuwa tatizo hilo ni kubwa sana kutokana na kesi nyingi za ukatili kuwa zimekwisharipotiwa ambazo takribani ni kesi 6000 ndani ya miezi 6 tu huku kesi nyingine nyingi zikiwa bado hazijaripotiwa.

”Kumpiga mwanamke kikatili ni moja ya tamaduni yetu hapa Papua New Guinea, huwa tunatumia kisu, bastola na kumtishia ili aweze kutusikiliza na kufanya kile tunachotaka kama wanaume.”

”Nimewahi kumtishia mke wangu bastola na ilibakia kidogo ni mfyatulie risasi kabisa lakini bahati mbaya nilifyatua katikati ya miguu yake”. alisema mwanaume mmoja.

Wanaume hao walipoulizwa kuwa wanawapenda wake zao walijibu wanawapenda ila tu wanataka wake zao kuwasikiliza na kufanya tu kile wanachotaka wao kufanya na ni lazima wapate ruhusa kwa waume zao ndio wafanye na sio kufanya kile wanachokitaka wao.

Aidha wanawake wa mji huo wameonekana kutokuwa na furaha na wamesema ni lazima wapambane kumaliza ukatili huo unaofanyika dhidi yao kwani hawapo tayari kuona watoto wao wanaishi katika maisha hayo ya vitisho, wapo wanawake waliotoroka kabisa mji huo na kwenda kuishi sehemu nyingine kwa ajili kupata amani.

Nchini Tanzania ukatili wa kijinsia umekuwa ukipigwa vita katika maeneo tofauti ikiwemo serikali, taasisi za Kidini na Asasi mbalimbali, ambapo hivi karibuni Askofu wa Jimbo Katoliki la Tanga Mhashamu Thomas Kiangio alitaka hatua kali zichukuliwe kwa wanaohusika na kufanya vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa watoto ili kukomesha tabia hiyo kwenye jamii.

Aliyasema hayo wakati wa Ufunguzi wa Jubilei Kuu 2025 kwa waandishi wa Habari Jimbo Katoliki la Tanga ambapo alisema kwamba vyombo vya habari havipaswi kukaa kimya badala yake wawe mstari wa mbele kuwafichua wanaofanya vitendo hivyo.

Mhashamu Kiangio alisema kwa sababu pale ambapo vyombo bua habari vinapokaa kimya uovu unapotendeka watakuwa hawana maana yoyote ya uwepo wao kutokana na kusambaza taarifa nzuri kuacha mabaya yatendeka.

“Ukiangalie leo hii watoto wadogo wanahujumiwa wanaingizwa kwenye mifuko ya rambo vyombo vipo wapi na je wanatoa taarifa watoto wanatendwa ukatili wanauwawa wasiokuwa na hatia “alisema

Hata hivyo alisema kwamba wakati mwengine unasikia watoto wamepakiwa kwenye basi wanasafirishwa kuelekea mahali fulani wengine wapo hai wengine wamekufa lakini hawaona hatua wanayotenda kwa watu hao hivyo kuna umuhimu hatua kuchukuliwa.

“Wakati mwengine wanahabari wanatuletea taarifa za uchungu lakini hamtuambii aliyefanya hivyo ni nani na hatua gani zimechukuliwa kuweza kudhibiti vitendo vya namna hiyo kuendelea kwenye jamii” Alisema

Aidha alisema suala hilo lazima wao kama wanahabari walitafakari hasa ikiwa ni hija ya wanahabari kwamba wale ambao wanawatendea mabaya ya kuwaua watu wasiokuwa na hatia wafichuliwa na watoa taarifa kamili na wasitoe nusu nusu ili kuwezesha kukomesha vitendo hivyo

“Wana habari mnakazi kubwa sana na ndio maana Baba Mtakatifu akaifanya siku ya leo duniani ya wana habari kutokana na umuhimu wenu hivyo msiwe waongo mtoe taarifa watuhumiwa



# WENYE FEDHA ZAO NDIYO WATAKAOPATA URAIA MAREKANI

NA MWANDISHI WETU

RAIS wa Marekani Donald Trump ametangaza mipango ya kuanzisha 'viza ya dhahabu' inayogharimu dola za kimarekani milioni 5, ambayo inatoa ukaazi wa kudumu na njia ya kupata uraia kwa raia matajiri kutoka nchi za kigeni.

"Watakuwa watu matajiri na watakuwa na mafanikio, na watakuwa wakitumia pesa nyingi, kulipa kodi nyingi, na kuajiri watu wengi. Tunaamini itakuwa na mafanikio makubwa," Trump alisema katika Ofisi yake siku ya Jumanne.

Howard Lutnick, Waziri wa Biashara wa Marekani, amesema "vixa ya dhahabu" itachukua nafasi ya mpango wa sasa wa viza ya wawekezaji ya EB-5 – mpango ambao hutoa viza kwa wawekezaji wa kigeni. Uondoaji wa viza utazinufaisha vipi Tanzania na DR Congo?

Huku idadi ya viza za EB-5 zikiwa zimepungua, Trump amependekeza kuwa serikali ya shirikisho inaweza kuuza "viza za dhahabu" milioni 10 ili kupunguza nakisi.

Alipoulizwa na waandishi wa habari ikiwa Warusi matajiri wanaweza kupata viza hiyo, Trump alijibu: "Ndiyo, inawezekana. Ninawajua matajiri wa Kirusi ambao ni watu wazuri sana."

Hata hivyo, Lutnick alisema waombaji wote watafanyiwa uchunguzi wa kina ili kuhakikisha kuwa ni "wananchi wazuri, wa kiwango cha kimataifa."

Pia haijulikani ni muda gani wenye viza ya dhahabu watalazimika kusubiri ili kupata uraia.

Watu wenye 'kadi ya kijani' (green card) ikiwa ni pamoja na wanufaika wa mpango wa sasa wa EB-5 - kwa kawaida wanapaswa kuishi kama wakazi halali wa kudumu nchini Marekani kwa miaka mitano kabla ya kustahiki uraia.

Congress huamua sifa za uraia wa Marekani, lakini Trump anasema "viza ya dhahabu" hazitahitaji idhini ya bunge.

Maelezo ya mpango huo mpya yatatolewa baada ya wiki mbili, aliongeza.

Waziri wa Biashara wa Marekani, Howard Lutnick

Kulingana na Bw Lutnick, "programu ya EB-5... ilikuwa imejaa upuuzi na ulaghai. Ilikuwa ni njia ya kupata kadi ya kijani ambayo ilikuwa ya bei ya chini. Kwa hivyo rais amesema, badala ya kuwa na aina hii ya programu ya EB-5, tutaondoa mpango wa EB-5."

Bunge la Marekani lilianzisha mpango wa EB-5 mwaka 1990 ili kuvutia uwekezaji wa kigeni. Hutoa fursa kwa watu binafsi kuwekeza takriban dola milioni 1 katika biashara inayounda angalau nafasi 10 za kazi.

***Utafiti wa viza ya dhahabu kwa Umoja wa Ulaya, uliofanywa na London School of Economics and Political Sciencena na Chuo Kikuu cha Harvard nchini Marekani pia ulitilia shaka mantiki ya kiuchumi ya miradi hii, na kuhitimisha kwamba iliwakilisha sehemu "ndogo" tu ya uwekezaji wa kigeni na faida "isiyo na maana" ya kiuchumi.***

Chini ya mpango huu, wawekezaji hupokea kadi za kijani na kisha uraia. Kinyume chake, waombaji wengi wa kadi ya kijani husubiri kuanzia miezi hadi miaka kadhaa ili kupata ukaazi wa kudumu.

Mpango wa EB-5 hutoa viza 10,000 kwa mwaka, huku 3,000 zikiwa zimetengwa kwa ajili ya wawekezaji katika maeneo yenye ukosefu mkubwa wa ajira, kulingana na serikali ya Marekani. Madhumuni yake ni "kuchochea uchumi wa Marekani kupitia uundaji wa nafasi za kazi na uwekezaji unaofanywa na wawekezaji wa kigeni."

Katika kipindi cha miezi 12 hadi tarehe 30 Septemba 2022, takriban watu 8,000 walipata viza za wawekezaji, kulingana na Takwimu za Uhamiaji za Idara ya Usalama wa Taifa.

Kwa kuongezea, mwaka 2021, Idara ya Utafiti ya Bunge la Marekani iligundua kuwa viza za EB-5 "zina hatari zaidi ya ulaghai" ikilinganishwa na viza vingine za wahamiaji.

"Hatari hizo zinahusishwa na ugumu wa kuthibitisha kuwa fedha za wawekezaji ni urahisi wa kutokea kwa upendeleo," ilisema ripoti hiyo.

Viza ya dhahabu na pasipoti ni maarufu kwa watu matajiri

Miradi kama hiyo ni ya kawaida duniani kote. Miradi ya "visa ya dhahabu" inawapa wageni matajiri haki ya kuishi na kufanya kazi katika nchi nyingine baada kuweka uwekezaji mkubwa.

Pia kuna mipango ya "pasipoti ya dhahabu", maarufu katika baadhi ya mataifa ya Karibea, watu matajiri hupata haki zote za uraia, ikiwa ni pamoja na haki ya kufanya kazi na kupiga kura katika nchi wanayoomba.

Henley & Partners, kampuni ya ushauri yenye makao makuu nchini Uingereza, inaripoti kuwa zaidi ya nchi 100 hutoa "viza ya dhahabu" kwa watu matajiri, ikiwa ni pamoja na Marekani, Uingereza, Hispania, Ugiriki, Malta, Australia, Canada na Italia.

Lakini, programu hizi zimekuwa chini ya ukosoaji na kuchunguzwa.

"Zinaweza kusaidia kuchochea ukuaji wa uchumi kupitia uwekezaji wa moja kwa moja, lakini pia zinavutia wahalifu na mafisadi wanaotaka kukwepa mikono ya sheria kwa mapato ya uhalifu yanayofikia mabilioni ya dola," kulingana na ripoti iliyochapishwa na Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo mwaka 2023.

Transparency International, shirika la kimataifa linalofuatilia rushwa katika zaidi ya nchi 100, linasema mpango huo katika nchi za Umoja wa Ulaya, "si kuhusu uwekezaji au uhamiaji – bali ni kuhusu maslahi ya rushwa."

Kumekuwa na ukosoaji kutoka mashirika mbalimbali ya Ulaya. Mwaka 2022, Kamati ya Umoja wa Ulaya kuhusu Uhuru wa Kiraia, Haki na Masuala ya Ndani ilipiga kura ya kupiga marufuku pasi za kusafiria za dhahabu.

Wasiwasi huu umesababisha nchi kadhaa za Ulaya, ikiwa ni pamoja na Uingereza, Uhispania, Uholanzi, na Ugiriki, kupunguza kasi ya programu zao za viza ya dhahabu katika miaka ya hivi karibuni.

Uhispania, kwa mfano, iliondoa programu yake ya "viza ya dhahabu" iliyoundwa 2013 ambayo ilitoa viza kwa wawekezaji walionunua mali yenye thamani ya pauni 500,000 ($525,000) au zaidi. Tarehe ya mwisho ya kutuma maombi ni tarehe 3 Aprili 2025.

Waziri Mkuu wa Uhispania, Pedro Sánchez alisema mwaka jana nia ya serikali yake ni kufuta mpango ili "kuhakikisha kuwa nyumba ni haki na sio suala tu la biashara."

Utafiti wa viza ya dhahabu kwa Umoja wa Ulaya, uliofanywa na London School of Economics and Political Sciencena na Chuo Kikuu cha Harvard nchini Marekani pia ulitilia shaka mantiki ya kiuchumi ya miradi hii, na kuhitimisha kwamba iliwakilisha sehemu "ndogo" tu ya uwekezaji wa kigeni na faida "isiyo na maana" ya kiuchumi.

Uchunguzi wa mtandao wa kimataifa wa waandishi wa habari wa uchunguzi - uliochapishwa Oktoba 2023 pia ulifichua kwamba kanali wa zamani wa Libya anayetuhumiwa kwa uhalifu wa kivita na mfanyabiashara wa Kituruki aliyehukumiwa kifungo nchini Uturuki waliweza kununua pasipoti ya Dominika kupitia mipango hii.



# NI KWELI NDOA ZA BINAMU HULETA WATOTO DHAIFU?-1



NA MWANDISHI WETU

UANI mwa nyumba iliyoko Bradford dada watatu wanaonekana wakipiga soga.

Mtaalam wa ulimbwende amekaa kwa kochi tayari kuwapamba warembo hawa.

Shangwe na nderemo zimetapakaa kila mahali kote chumbani.

Dada hawa wanajiandaa kwa harusi ya mmoja wa familia itakayofanyika mwishoni mwa wiki wiki, ambayo bibi na bwana harusi ni binamu.

Kwa wengi ndoa za aina hii zinawastaajabisha lakini kwa familia hii na baadhi ya maeneo ya Bradford ni kitu cha kawaida.

Ayesha mwenye umri wa miaka 28 ni mkubwa kuliko wenzake pia aliolewa na binamu yake miaka ya nyuma.

Kwasasa ana watoto wawili na anatuelezea anafurahia ndoa yake na haikuwa jambo geni kuolewa na binamu yake.

Mama yao mwenye asili ya Pakistani alifikiria mabinti zake wote watatu wataingia kwenye ndoa za aina hii.

Lakini Salina mwenye umri wa miaka 26, ambaye ni mdogo kuliko wote anasema alivunja dhana hii na kuolewa kwenye ndoa ya 'mapenzi', kwa kuchagua mwenza ambaye hawana uhusiano wowote wa kindugu.

Salina anatuambia hulka yake ni mchangamfu na aliyejaa maono , na kuolewa na binamu yake hakupendelea kabisa.

Kisha kuna Malika, dada aliyemfuata Salina kwasasa hana mchumba lakini ameapa hataolewa na mwanaume ndugu, kama binamu.

"Nilimwambia mama yngu, si wakejeli dada zangu lakini kuolewa na binamu hapana" Malika anatuarifu.

Anatueleza kupata elimu kumemfungua macho na kumpa fursa nyingi.

" Awali ingekuwa unaendelea na masomo ungejikuta bado unafikiria kuolewa lakini kwa sasa mambo ni tofauti".

Takwimu za kutisha

Uingereza na pia Ulaya ndoa za binamu zimeendelea kuangaziwa zaidi haswa na madaktari ambao wanaonya kuwa ndoa za binamu na ndugu wa karibu zaidi, watoto wanaozaliwa huwa na matatizo ya afya.

Na sasa kuna takwimu za kutamausha kutoka Bradford ambazo zinatonesha kidonda zaidi.

Wataalam katika Chuo cha mjini wanaingia katika mafunzo na tathmini mwaka wa 18.

Ni utafiti wa kiafya ambao ni mkubwa kuwahi kutokea .

Kati ya mwaka 2007 hadi 2010 walisajili watoto 13,000 ambao wamewafuatilia tangu wadogo mpaka kuingia wabaleghe.

Zaidi ya mmoja kati ya sita wanaofuatiliwa wazazi wao ni binamu, wengi wakitoka jamii ya Pakistani iliyoko Bradford na kuufanya utafiti huu kuwa muhimu zaidi kubaini athari za ndoa kati ya binamu.

Njia ya wazi ambayo wazazi wawili wanaoshirikiana damu wanaweza kuongeza hatari ya afya kwa mtoto ni kupitia ugonjwa wa kurithi, kama vile selimundu na uvimbe kwenye kizazi.

Kulingana na nadharia ya Gregor Mendel, ikiwa wazazi wote wawili wana jeni ya ugonjwa huo, kuna nafasi moja kwa nne kwamba mtoto wao atarithi hali hiyo.

Wakati wazazi ni binamu, kuna uwezekano mkubwa kwa wote wawili kuwa wana jeni za ugonjwa huo.

Mtoto wa binamu wa kwanza ana asilimia 6 ya uwezekano wa kurithi ugonjwa wa kimaumbile, ikilinganishwa na asilimia 3 ya mtoto aliyezaliwa na wazazi ambao sio binadmu.

Hata hivyo, utafiti wa Bradford ulitazama suala hili kwa mtazamo mpana zaidi na kutoa mwangaza mpya. Watafiti hawakuchunguza tu kama mtoto alikuwa na ugonjwa wa kimaumbile, bali walijumuisha data nyingi, zikijumuisha maendeleo ya usemi na lugha ya watoto, mara kwa mara ya huduma za afya, na ufanisi wao shuleni.

Walitumia mfano wa kihesabu kuondoa athari za umaskini na elimu ya wazazi, ili kujikita katika athari za "consanguinity," neno la kisayansi linalomaanisha kuwa wazazi ni wa familia moja.

Waligundua kuwa iwapo umaskini wa familia umedhibitiwa, mtoto wa binamu wa kwanza eneo la Bradford alikuwa na nafasi ya asilimia 11% kuwa matatizo ya kuzungumza, ikilinganishwa na asilimia 7% ya watoto waliozaliwa na wazazi ambao hawahusiani kwa damu.

Pia waligundua kuwa watoto waliozaliwa na binamu wa kwanza walitembelea mara nyingi hospitali kwa matibabu ukilinganisha na waliozaliwa kwa ndoa za kawaida - wanne licha ya watatu kila mwaka.

Neil Small profesa katika chuo cha Bradford na muanzilishi wa tathmini hiyo anasema iwapo watoto wote wanamatatizo ya kimaumbile walitembelea hospitali '' haimaniishi huduma za matabibu zinahitajika zaidi kwa watoto waliozaliwa na wanandoa ambao wanahusiana.''

Utafiti huu anasema '' ni muhimu kwasababu unatoa fursa ya namna ya kukabiliana na kulenga mikakati ya kuepusha na kutibu magonjwa yanayotokana na hali hii.''

Wasiwasi waibuka

Utafiti mmoja katika jamii moja ya Bradford haiwakilishi Uingereza kwa ujumla.

Hata hivyo, imeibua wasiwasi miongoni mwa wanasayansi ambao pia umechochea wabunge kufuatilia kiundani hasa Ulaya.

Kwa mfano, Norway, ndoa za binamu wa kwanza zilipigwa marufuku na nchini Uswidi , marufuku ya ndoa hizo yataanza kutekelezwa mwaka ujao.

Richard Holden amependekeza mswada wa kuharamisha ndoa za binamu akiongezea kwa orodha za ndoa zilizopigwa marufuku

Nchini Uingereza, mbunge Richard Holden amependekeza mswada wa kuharamisha ndoa za binamu akiongezea kwa orodha

>> Itaendelea toleo lijalo...

# Michezo Kimataifa


## Tetesi za soka



CHELSEA wanaamini wanaweza kufanya dili kwa ajili ya mlinzi wa Sporting Ousmane Diomande msimu wa joto - chini ya kipengele cha ukubwa wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast mwenye umri wa miaka 21. (TeamTalk),



JUVENTUS wameipa Chelsea ruksa ya kumsajili kiungo wa kati wa Brazil Douglas Luiz, 26, ambaye pia ananyatiwa na Manchester City na Arsenal, hii imetokana na mazungumzo mazuri kati ya klabu hizo na pia maslahi yaliyoridhiwa na pande hizi mbili.





1

MSHAMBULIAJI wa Uruguay Darwin Nunez, 25, mwezi Januari aliiambia Liverpool kuwa anataka kukihama klabu hicho lakini ombi lake la kujiunga na klabu ya Al-Hilal ya Saudia lilipingwa. (Football Insider)

BAADA ya kulaulimiwa kwa muda mrefu kuwa tatizo la Arsenal ni kudharau kufaya usajili hasa eneo la ufungaji, hatimaye klabu hiyo imesikia kilio hicho na sasa imeanza mawindo makali ili kutibu pengo lililopo, kufutia mkakati huyo klabu hiyo imeingia chimbo na kumnasa Straika makali Raia Slovenia anayekipiga katika klabu ya RB Leipzig ya Ujerumani





## KASEJA APEWA KIBARUA KIZITO KAGERA SUGAR

NA MWANDISHI WETU

KWA mara ya kwanza kipa maarufu nchini Juma Kaseja atasimama kama Kocha Mkuu akijaribu kukinusuru kikosi cha timu kongwe katika Ligi Kuu Kagera Suga,r isishuke daraja msimu huu.

Kaseja alikabidhiwa mikoba hiyo juzi na uongozi wa klabu hiyo yenye makao yake makuu mjini Bukoba, huku msimamo ukisoma kuwa ipo nafasi ya 15 katika msimamo wa ligi ikiwa ni ya pili kutoka mwisho.

Mpaka sasa Kagera imeshacheza mechi 22 ikishinda 3 na kutoka sare 7, kibindoni ikiwa na ponti zake 16 pekee.

Nafasi hiyo si salama sana kwa Wana 'Nkurukumbi' hao kwani Ken Gold iunayoburuza mkia ina jumla ya pointi 15 pungufu ya moja tu kuwa sawa na Kagera Sugar, huku timu iliyo juu ambayo nayo ipo katika zile tatu zilizopo katika mstari mwekundu ni Tanzania Prisons ambayo imecheza mechi 22 na kujikusanyia Pointi 18, nyongeza ya pointi mbili kutoka kwa Kagera.

Kwa vyovyote Juma Kaseja aliyewahi kuwa kipa mahiri wa vikosi vya Simba na Yanga pamoja na timu ya taifa hatokipokea cheo hicho kwa furaha kwani itambidi kupambana ili ainasue timu hiyo kutoka mkiani, ili aweze kuwa na uhakika wa kurudi tena kucheza Ligi Kuu ya NBC msimu ujao.



# SIKIA KISA CHA TALAKA INAYOSISIMUA - 2

NA MWANDISHI WETU

MFALME wa Jamii ya Wazulu anayefahamika kama 'Simba wa taifa,' ndiye mwenye kuhifadhi tamaduni za jamii hii ambazo ni za jadi. Tamaduni hizi zimedumisha ndoa na hususan ndoa ya wake wengi kama jambo kubwa kabisa la mafanikio ya ufalme.

Na japo majukumu yake nchini Afrika Kusini ni ya kitamaduni na hayana uzito katika sheria za nchi hiyo, kiongozi huyu wa jamii anasalia kuwa na ushawishi mkubwa katika jamii huku ofisi yake ikipokea ufadhili wa mamilioni ya dola za Kimarekani kutoka kwa serikali kuu.

Mfalme huyo ambaye alikulia katika taifa jirani la Eswatini , alipata masomo yake nchini Marekani na kukabidhiwa wadhifa wa uongozi mnamo 2021. Aidha amekuwa akikabiliwa na utata tangu awali.

Kukabidhiwa kwake mamlaka kulipingwa mahakamani na kaka yake mkubwa ñ ambaye ni wa mama mwingine ñ aliyetaka kupokezwa ufalme huo.

Ndoa yake ya pili, imegonga vichwa vya habari, na jaribio lake kuoa mke wa tatu limegongwa mwamba huku kukiwa na ripoti kwamba ana uhusiano kwa kando na mwanamfamle wa kike.

Hata hivyo, kashfa inayozunguka maisha ya kiongozi huyo mwenye umri wa miaka 50 imekuwa ikijadiliwa chini kwa chini ñ hadi pale alipotangaza azma ya kumtalaki mke wake na kuwasilisha ombi rasmi mahakamani mwezi Desemba.

Profesa Madibuko amekiri kwamba kumbukumbu za historia ya Wa Zulu zinaonyesha kwamba kuna mfalme ambaye katiak karne ya 20 alimtalaki mmoja wa wake zake , ' ila hilo lilifanyika kimya kimya na kuwa siri kubwa katika familia hiyo ya kifalme,' ikizingatiwa kwamba talaka katika ufamle wa zulu sio jambo la kawaida.

'Ikiwa uhusiano utavunjika, basi mke huyu ataendelea kuishi katika boma la mfalme. Atapewa eneo lake kando, na hatakuwa na uhusiano an mfalme , ila yeye na watoto wake watatunzwa.'

Mama Myeni na Mfalme Misuzulu KaZwelithini. Chanzo cha picha,KwaZulu-Natal

Maelezo ya picha,Mfamle huenda ameahirisha ndoa yake ya mke wa tatu Nomzamo Myeni, ila wapenzi hao walionekana pamoja katika hafla ya kitaifa.

Ilikuwa muda kabla ya kupokezwa ufalme ñ punde tu baada ya kifo cha ghafla cha baba na mama yake miaka minne iliyopita ñ kwamba mwanamfalme (wakati huo) Misuzulu alipomuoa Ntokoto Mayisela.

Wawili hao walikuwa tayari kwenye uhusiano wa kimapnenzi na walikuwa tayari ni wazazi wa Watoto wawili , ila kwa mujibu wa mtaalamu mwingine wa utamaduni wa jamii ya Zulu, Prof Muza Xulu kutoka chuo kikuu cha Zululand, uamuzi wa kufunga ndoa ulionekana kuharakishwa.

'Ilionekana kwamba mwanafalme hangeweza kuwa mfalme ikiwa hakuw ana mke,' alioambia BBC.

Malkia kaMayisela alitokea familia ya kawaida ñ kama wake wengine wa wafalme wa Kizulu ñ kutoka mji mdogo wa uchimbaji madini katika jimbo la KwaZulu ñ Natal.

'Malkia alimvutia Mfalme katika mgahawa mmoja kwenye mji wa pwani wa Durban alipokuwa akifanya kazi kama muimbaji,'alisema Prof Xulu.

Hadhi yake katika familia iliwekwa wazi wakati wa kutawazwa kwa mfalme mnamo Desemba 2022 alipoketi kando yake.

Ila nafasi yake sasa inatishika , anapotaja Mume wake kwamba wawili hao hawajaishi pamoja kama mume na mke kwa mwaka mmoja uliopita na kwamba ndoa yao imevunjika.

Kasri ya mfalme ilifuatilizia matamshi yake kwa kutuma mualiko wa ndoa ya Mfamle kwa mke mwingine, Nomzamo Mayeni mwishoni mwa mwezi Januari . Mahari ya bibi harusi inayofahamika kama LOBOLA kwa lugha ya kizulu imeshalipwa ñ huku ng'mbe wanaothaminiwa sana katika jamii hiyo wakitolewa kama mahari.

Malkia kaMayisela hajapokea haya yote vyema, akitaja kwamba huenda akawasilisha malalamishi ya kutaka ndoa hiyo kutofanyika , hali iliyosababisha ndoa hiyo kuahirishwa.

Ameiambia mahakama kwamba , mfalme ambaye anatambulika miongoni mwa jamii hiyo kama "ingonyama", kumaanisha simba, angekuwa anavunja sheria za ndoa kwa kufunga ndoa ya pili japo mke wa kwanza yupo. Anasema pia kwamba hatua hiyo inafanyika chini ya ndoa iliyofanyika katika ofisi ya mwanasheria mkuu ambayo haikubaliwi kuwa na wake wengi na kwamba kabla ya kuendeela mbele anapaswa kubadilisha ndoa yake ya kwanza kuwa ya kitamaduni kama inavyofanyika chini ya tamaduni za jamii ya wazulu.

Jaji alitupilia mbali ombi hilo kwa kusema kwamba ,malkia huyo alikuwa nabadili maoni yake baada ya kukubali kwamba mume wake angekuwa na wake zaidi ya mmoja awali.

Alisema kwamba mfalme alikuwa tayari ameshaoa mke wa pili ñ Nozizwe kaMulela ambaye ni mkurugenzi mkuu wa benki ya Eswatini mnamo 2022.

Nozizwe kaMulela, mfanyakzi katika benki kutoka Eswatini, anaonekana kuwa mwenza mzuri wa mfalme na baadhi.Chanzo cha picha,-Supplied

Maelezo ya picha,Nozizwe kaMulela, mfanyakzi katika benki kutoka Eswatini, anaonekana kuwa mwenza mzuri wa mfalme na baadhi.


Prof Mazibuko ameseka kwamba ndoa yenye wake wengi haikuwa jambo ambalo lilifanyika sana katika jamii ya WaZulu, kwani wafalme wawili wa kwanza hawakuwahi kuoa.

Ila ndoa yenye wake wengi ilikumbatiwa na wafalme waliofuatia ñ Mfalme Misu-

>> Itaendelea toleo lijalo...



JAMVI LA HABARI
SPOTI
ALHAMISI MACHI 06, 2025



**Nicole Berry akamatwa kwa utapeli**

>> Soma Uk. 15

# TIKETI MECHI YA SIMBA, YANGA ZAADIMIKA MTAANI



NA MWANDISHI WETU

WAKATI zikisalia siku mbili kabla ya kufanyika mpambano wa kihistoria kati ya timu pendwa za Tanzania, Simba na Yanga kasi ununuzi wa tiketi kwa ajili ya mchezo huo inakwenda mbio za nyikani.

Hadi kufikia jana asubuhi kupitia ukurasa wa Yanga ilitambusha kununuliwa kwa tiketi zote za VIP na hivyo mashabiki wakaanza kuhamasishana ili kuzifagia zilizobaki.

Tiketi zilizokuwa zikiendelea kununuliwa kwa kasi tangu jana ni pamoja na VIP B, C, Orange na Mzunguko, ambapo gazeti hili halijapata taarifa mpya kama zilienndelea kuwepo katika vituo au zilishamalizika

Mchezo huo unaovuta hisia kwa mashabiki wa soka nchini, unatarajiwa kupigwa katika dimba la Mkapa majira ya saa 1:00 usiku.

## Simba SC yamtolea macho mwamuzi

NA MWANDISHI WETU

HAKUNA ubishi kwamba Simba na Yanga ni rasmi sasa zitaonyeshana ubabe katika mchezo wa Ligi Kuu ya NBC, utakaopigwa Jumamosi Machi 8, huku mwamuzi wa mchezo huo akitajwa kuwa ni Ahmed Arajiga.

Refa huyo kutoka Manyara atakuwa akiandika rekodi ya kuchezesha mechi ya watani hao mfululizo baada ya kufanya hivyo katika mechi tatu zilizopita.

Muda mfupi baada ya Bodi ya Ligi kumtaja Arajige kama



mwamuzi wa kati katika mechi hiyo, mashabiki wa timu hizo wamelipokea jina hilo kwa hisia tofauti, huku wale wa Simba wakionyeshwa kutoridhishwa, huku wenzao wa Yanga wakilifagilia.

Hata hivyo hakuna sababu inayotolewa na mashabiki wa Simba dhidi yake, badala yake Wekundu hao wa Msimbazi wanadai kutokuwa na bahati naye, licha ya kusifu uwezo wake.

Ikumbukwe Arajiga ndiye aliyepuliza kipyenga wakati Yanga ilipovuna kalamu ya ushindi wa mabao 5-1 dhidi ya Simba na hata ushindi wa mabao 2-1.



## Kaseja apewa kibarua kizito Kagera Sugar

**KWA MARA** ya kwanza kipa maarufu nchini Juma Kaseja atasimama kama Kocha Mkuu akijaribu kukinusuru kikosi cha timu kongwe katika Ligi Kuu Kagera Suga,r isishuke daraja msimu huu.

>> Inaendelea Uk. 14

GAZETI HILI HUTOLEWA NA JAMVI MEDIA GROUP, S. L. P 78862, DAR ES SALAAM